SHEIKH: HASSAN MUSA SAFFAR

قوانين الزواج - اللغة السواحيلية . كينيا . ممباسا ٢٠٠٧

# Ndoa

# Hukmu na Malengo yake

© Sheikh Hassan M. Saffar

Kimechapichwa na:

Sh. Hassan Musa Saffar
P.O. Box 1322
Qatif 31911

Tel: + 9663855521

Fax: + 966385126

Website: www.saffar.org
Email: office@saffar.org
Saudi Arabia

Kimefasiriwa na:

Ustadh K. Kea
Mombasa
Kenya

Mhariri:

A. Mohamed
2007 A.D.

# KANUNI ZA NDOA

Imefasiriwa kutoka kwenye kitabu:

*Qawaaninu - Zawaaj*

Sheikh Hassan Saffar

**YALIYOMO**


UTANGULIZI ........................................................................i

BAINA YA NDOA NA KUINGILIANA................................1

Mila na desturi .............................................................1

Maana ya kuingiliana (Dukhuul) ...................................2

Talaka kabla ya Dukhuul..............................................3

Kufariki kabla Dukhuul.................................................4

Haki za mume na mke kabla ya Dukhuul ............................4

KUVUNJA NDOA .......................................................7

Vitu vinavyopelekea kuvunja ndoa .................................8

Hukmu za kuvunja ndoa...................................................9

Baina ya kuvunja ndoa na talaka....................................10

MKE KUTAKA KUVUNJA NDOA .................................11

Mambo yanayopelekea kuvunja ndoa (upande wa mke)...12

Kujua kabla ya ndoa.........................................................13

Kupoteza nguvu za kiume baada ya kuingiliana................13

Udanganyifu na kuvunja ndoa .........................................15

Namna za udanganyifu....................................................17

Kuchukua hatua ya kuvunja ndoa ...................................18

MAONI YA MADHEHEBU YA SUNNI ............................19

USIKU WA MAHARUSI NA KUINGILIANA...................21

CHAKULA CHA HARUSI (WALIMA) .............................23

Sherehe za usiku ya maharusi 'zafaaf'...............................24

Yaliyopendekezwa siku ya maharusi.................................25

Kusherehekea harusi .......................................................27

Nyimbo wakati wa harusi.................................................28

Wanaosema kwamba yafaa ...............................................31

Kuwachosha maharusi wawili..........................................32

Ndoa ya jumuia ...............................................................33

## UTANGULIZI

Hakika ipo haja kubwa ya kudhurisha ndoto na malengo ya Uislamu na kusambaza mipango yake, maelezo na sheria zake juu ya mambo ya kifamilia kulingana na kiwango cha ulevi cha jamii ya mwanadamu kwa sura ya kijumla na kwa kiwango cha muungano wa jamii ya kiislamu kwa sura mahsusi ili jamii iwe na uwezo wa kujichagulia kinyume na ile dasturi ya ki-magharibi.

Na haja yote yanahitaji kuyabadilisha kutoka katika elimu iliyoganda na kuanza kuyaeleza kiujuzi na kwa uwazi.

Na tumegundua kwamba maelezo ya dini na sheria za Kiislamu juu ya familia na mambo yanayohusu, imekuwa ni kawaida katika kuandikwa katika vitabu vya dini na fiqh kwa lugha ya kielimu mahsusi, na kwa mfumo na njia ambayo haiwezi kufanywa upya na kugeuzwa kimaendeleo. Na hata vitabu vya fatwa (hukmu) vinavyoandikwa na wanavyuoni wa fiqhi mara nyingi vimekosa mambo hayo mawili (kufanywa upya na kugeuzwa kimaendeleo).

Na kwa ajili havimvutii mwanadamu wa leo anaetarajia maendeleo wala msomaji hawezi kupata ubainifu kwa uwazi.

Na katika utafiti wangu wa dini juu ya mambo ya jamii ambayo mengi yanafungamana na mambo ya familia kama vile kusaidia katika maudhui ya ndoa, upitishaji wa ndoa, kuachana (talaka), kupatanisha waliotengana, kutatua matatizo ya kinyumba, kufuatilia mambo ya kueleimishana, kufungua mawazo ya vijana na kuangalia mafungamano yao na jamii zao katika hali hiyo basi nimegundua kuwa kuna upungufu na mwanya mkubwa katika kuuamsha ulimwengu na kuelemisha kwa mafunzo ya kiislamu na sheria zake katika nyanja hizi, ambayo yataweza kufunguwa uwanja mpana wa kupokea mafunzo kwa njia ya mawasiliano ambayo yanaweza kubadilisha desturi ya maisha ya ki-magharibi ambazo huwenda hazikubaliani na maoni ya kidini.

Jambo hili ndilo lililo nipeleka kusoma mambo ya kifamilia katika fiqhi ya Uislamu na kutanguliza niliyoyapata kwa jamii tena kwa lugha ya kielimu ya kileo iliyo wazi na rahisi kueleweka.

Hakika nilianza juu ya utafiti huu kupitia darasa za kila wiki (ijumaa) zinazohudhuriwa na kundi la wasomi kila siku ya alhamisi tangu wakati wa kiangaza mwaka 2000A.D. (1421 H). Darasa hizi zilikuwa ni kwa njia ya maswali na kujadiliana, utafiti wangu nilikuwa nikiuandika baadaye na kuchapisha matoleo kadha wa kadha kwa kukusanya kutoka kwa wanavyuoni watukufu na vijana wasomi ili nipate kunufaika na maoni na rai zao mpaka nikafikisha vikao 50 vya darasa nilizoziandika zote, nikaona nizikusanye zote na kufanya kama juzuu ya kwanza ya utafiti huu. Na ninatarajia uwezo kwa Mwenyezi Mungu wa kuendeleza darasa na kutafiti yaliyobakia juu ya fiqh ya familia katika mawazo na sheria ya Uislamu.

Na imenilazimu katika utafiti wangu kutumia muelekeo wa fiqh kwa kulinganisha maoni ya madhehebu tofauti ya Kiislamu na kutumia vitabu vinavyotegemea na kila madhehebu na pia *Encyclopedia* za kifiqhi zilizo maarufu na kuchunguza sana kila rai na kuihakikisha kupitia vitabu kimetolewa rai hiyo.

Na ikanijia kwa uwazi ukuruba na kuingiliana kati ya maoni ya wanavyuoni wa fiqhi wa kiislamu juu ya kutofautiana kimadhehebu, hakika ni kwamba wanakubaliana juu ya mambo ya kimsingi ya kisheria na tafauti kati yao inapatikana katika mambo yaliyozaliwa na misingi na katika ufafanuzi. Mara nyingi unaweza kupata wanavyuoni wa fiqhi upande wa shia wakitafatiana na wenzao katika baadhi ya mambo na maoni yao yakawa ni sawa na yale ya dhehebu la sunni, na vile vile pia upande wa Sunni kutafautiana na sunni wenzao na kukubaliana na Sshia. Na msomaji mtukufu atapata katika utafiti huu mifano inayorudiwa rudiwa juu ya ukweli wa jambo hili.

Na huenda nikataja baadhi ya niliyo ya shuhudia na matukio yanayotokea katika jamii ninayoishia ili kuyapa mawazo uhai wa kimatukio.

Hakika nimejitahidi kulifahamu somo la fiqh na kuandika kwa lugha ya kileo iliyo wazi na kuitanguliza kwa maoni ya kiujuzi ya kijamii.

Namuomba Mwenyezi Mungu aikubali bidii hii yangu na malengo yake yawe ni yenye manufaa katika matumizi ya sheria ya kiislamu na kutengeza tabia katika jamii.

Kama vile ninavyotarajia kufaidika na maoni na rai za wanavyuoni watukufu na wajuzi ili kuendeleza utafiti na kuziba upungufu na mwanya.
Ninamuomba Yeye alietukuka uwezo wa kumtumikia Yeye na dini yake, na hilo liwe ni kwa ajili ya utakaso wake. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mlezi wa walimwengu.

## BAINA YA NDOA NA KUINGILIANA

Pindi tu ndoa inapopita kisheria, watu wawili huwa ni bibi na bwana na inafuatia baada ya hapo uwajibikaji na haki za kutendeana kati ya mume na mke.

Mbeleni walikuwa maharusi wanaingilia maisha yao ya kindoa yanayowahusisha wote wawili punde tu baada ya ndoa. Na baadhi ya jamii za kiislamu bado ziko katika utaratibu huu. Lakini ilivyozoelekea sasa katika jamii nyingi ni kuwepo kwa muda kidogo kati ya kupitishwa ndoa na sherehe za harusi na pia kumuingilia mwanamke. Hili ni kwa ajili ya kupunguza mahitaji ya kimaisha ya kifamilia kama vile kukamilisha malazi, vyombo vya nyumbani ambapo vijana wengi hawawezi kudhamini mahari, kusimamia gharama za harusi na sherehe kwa wakati mmoja.

Kwa upande mwengine: Muda huu uwe kama nafasi kwao wao ya kupata kutambuana na kujiandaa kwa maisha ya mume na mke. Kabla ya ndoa hakuna sheria inayoruhusu wao wawili kukutana na kutambuana kwa undani kati yao. Na iwapo watahitaji kuonana ili kila mtu aridhike na mwengine basi ni wakati wa kuposa pakiwa na watu, na hili la uposi hufanywa kabla ya ndoa.

Na muda huu wa kufahamiana baada ya ndoa unahitajika kuwa mfupi kama miezi miwili ama mitatu, muda huu unatosha kabisa kutambuana vyema na kujiandaa kimaisha.

### Mila na desturi

Baadi ya familia hawapendi kuanzisha mafungumano kikamilifu kati ya mume na mke baina ya muda wa ndoa na kabla ya kuingiliana. Na wanaona kuwa kuweko uwazo wa mafungamano kati ya hao wawili kwa wakati huo ni jambo la aibu kijamii na ni ishara upungufu wa heshima kwa mwanamke na adabu. Na pia kuhofia kuwepo mafungamano ya kikamilifu kati ya mume na mke kabla ya usiku wa maharusi.

Kisheria hapana makosa kuweko mafungumano ya uwazi kati yao kwa maana huwa ni tayari kama mume na mke baada ya kupita ndoa na wana haki za kikamilifu.

**Maana ya kuingiliana (*Dukhuul*)**

Maana ya *Dukhuul* kulingana na uwelevu wa watu ni harusi na sherehe zake zote na kushikanisha mke na mume kuishi pamoja.

Ama maana yake kisheria ni tendo la kuingiliana kimwili na kuweko kwa ukaribu kijinsia baada ya ndoa iwe sherehe ya harusi imefanyika ama la.

Basi iwapo watapata kujitenga na watu na kuingiliana kimwili basi mwanamke anastahili kupewa mahari kamili na atakaa eda iwapo ataachwa na anaweza kurejewa akiwa kwenye eda ya kuachwa.

Na lau itapita ndoa na kusipatikaniwe starehe zozote kimwili basi huyo hajaingiliwa kwa sababu Aya tukufu inasema "Kabla ya kuwagusa (wanawake)" na kuwagusa katika Aya hii inamaanisha kuwaingilia kimwili.

Imepokewa kwa Imam Jafar Sadiq (a.s.) akisema "Zitakapogusana tupu mbili basi ni lazima kutolewe mahari kamili na kukaa eda."

Na imepokewa kutoka kwa Yunus bin Yakub akisema: "Nilimuuliza babake Abdallah yaani Imam Sadiq (a.s.) juu ya mtu alieoa, na akajifungia mlango na mkewe, akamshikashika na kumbusu lakini asimuingilie kimwili kisha akumuacha katika hali hiyo. Imam (a.s.) akasema: Basi mtu huyo atatoa nusu ya mahari waliyosikizana."

Na haya ndio maoni yanayofahamika zaidi katika wanavyuoni wa Shia na pia wafuasi wa Malik na Shafi, lakini baadhi ya wanavyuoni washia waliotangulia na wa Hanafii na Hambali wanasema kuwe kuwa pweke na mwanamke na kusiwe na pingamizi yoyote ya kuwazuia wao wasiingiliane, basi ni sawa na hukumu ya kuingiliana, kwa hiyo mahari ni

lazima itolewe kamili na mwanamke atakaa eda atakapoachwa na mume anaweza kumrudia akiwa kwenye eda.

Na akapokea Imam Ahmad bin Hambal na Athram kwa upokezi wao kutoka kwa Zararati bin Aufaa kuwa amesema: "Waliamua makhalifa kwamba mwenye kuufunga mlango wake ama akashukisha pazia basi ni lazima atoe mahari na mke atakaa eda atakapoachwa."

Na ikanukuliwa kutoka Ahmad bin Hambal kwamba, mtu akimbusu au kumkumbatia mkewe hata bila ya kuwa peke yao ni lazima atoe mahari kamili.

**Talaka kabla ya *Dukhuul***

Wakati mwengine hutokea kutokubaliana kati ya bibi na bwana baada ya ndoa. Ima kwa sababu ya kutambua mmoja wao kuwa sivyo alivyoelezwa kuhusu mume ama mke, au kukatokea utesi na wakaamua kuachana ama mmoja akasisitiza juu ya talaka.

Hakika talaka ni halali inayochukiza Mwenyezi Mungu lakini kutokea kwake kabla ya kuingiliana na kupata watoto huwa haina madhara makubwa.

Basi atakapomuacha mtu mkewe kabla kuingiliana basi ampe nusu ya mahari waliyokubaliana ila atakapoisamehe mke mahari hiyo ama baadhi yake ama msimamizi wake kulingana na mipaka ya maslahi ya mke.

Na mwenye kuachwa kabla ya kuingiliwa hakai eda na anaweza kuolewa na mume mwengine punde tu akiachwa.

Na talaka hiyo ni talaka *baain* yaani hawezi kurudia ila baada ya kufunga ndoa upya.

**Kufariki kabla *Dukhuul***

Mume anapofariki basi inamlazimu mke kukaa eda ya kufiwa na mumewe ambayo ni miezi minne na siku kumi hata kama atafariki kabla ya kumuingilia. Na iwapo atafariki ima mume ama mke kabla ya kuingiliana basi kuna mapokezi mengi yaliyopelekea kutafuatiana kimaoni wanavyuoni wa fiqhi juu haki ya mahari kwa mke. Kuna mapokezi matatu:

1. Ni lazima mke apewe mahari kamili iwapo atafariki yeye au mume kabla ya kuingiliana na maneno haya ndiyo yenye nguvu kwa wanavyuoni wa Shia na Sunni.
2. Mke anafaa kupewa nusu ya mahari waliosikizana. Na maneno haya pia baadhi ya wanavyuoni wa Shia wameifuata kama vile Sayyid Sistaany miongoni mwa wanavyuoni wa sasa.
3. Hukmu mbili kati ya kufa mume ama mke. Mume atakapofariki basi mke anafaa kupewa mahari kamili, na iwapo mke atafariki basi mume atowe nusu ya mahari waliosikizana.

Ama kwa upande wa urathi basi watarithiana kama mume na mke ilivyo kisheria atakapofariki mmoja wao baada ya kuingiliana.

**Haki za mume na mke kabla ya *Dukhuul***

Baada ya ndoa mume na mke wanaowajibika kutekelezana haki. Mke anawajibika kumstarehesha mumewe na asiwe mwenye kutoka bila ya ruhusa kutoka kwa mume wake. Na mume ni amsimamie mke kimaisha na akae nae kwa wema.

Lakini kimila na mazoefu ziko juu ya kuyaharikisha mahitaji haya kati ya mume na mke punde tu baada ya ndoa mume na mke huishi nyumba moja na mume kuanza kumsimamia mke

kimahitaji yote.

Ama kabla ya kuingiliana na kuwa pamoja rasmi, na kwamba kuharikisha hilo hakuwi ila kwa kukubali mume basi mke si makosa kutoka nyumbani bila ya ruhusa ya mumewe.

Na uwazi ni kuwa ni lazima amuangalie kimaisha katika muda huu wa ndoa na kuingiliana ili pakiwa na kitu cha kisheria kitakachozuia hilo.

Na wamelazimisha wanavyuoni wengi wa Sunni kwa mume kumsimamia mke kimaisha ila atakapokataa yeye mwenyewe ama walii wake kwani Mtume (s.a.w.) alimoa Aisha na akamuingilia baada ya miaka miwili na wala hakumsimamia kimahitaji ila baada ya kumuingilia, na wala hakuwajibika kumlipa kwa siku zilizopita.

Na wakati mwengine mume humuhitaji mke wake kutenda tendo la kijinsia baada ya ndoa na kabla ya kuwa pamoja rasmi na hili ni haki yake kisheria; lakini jambo hilo iwapo litakuwa ni uzito kijamii basi mke ana uwezo wa kukataa wakati ule madamu anajiandaa kwa kuingiliana naye watakapokuwa rasmi.

## KUVUNJANDOA

Kwa ajili ya kudumisha maisha ya mume na mke na kufikilia malengo yake, hapana budi kuwe na uwazi na kuridhika kutoka pande zote mbili. Iwapo mmoja wao atakuwa na kasoro ya kimwili ama kiakili na mwengine alikuwa hajazigundua ila hizi na kuridhika nazo, hilo linamaanisha kuwepo kwa kutoridhika na kutokubali kutoka kwa upande wa mume.

Kwa ajili hii Uislamu umeweka uwezo wa kuvunja ndoa ima kwa mke au mume atakapogundua kuwa kuna ila kwa mwenziwe baada ya ndoa kupita, wanavyuoni wengi wa kiislamu wasema hivyo, lakini Dhaahiriya wakasema kinyume cha hilo.

Na Shaukani aliyakubali na meneno haya na kuyatilia uzito.

Na ijapo mapokezi mengi katika vitabu vya shia kutoka kwa maimamu wa Ahlul bait (a.s.) yanayothibitisha usawa wa kuvunja ndoa kwa ajili ya kupatikaniwa ila kwa mmoja. Na wanavyuoni wao wakayakubali maneno haya na kuyafanya hoja kwa kuyachukulia kuwa ni miongoni mwa Sunnah.

Na Hanafii wakasema kuwa: "Uwezo wa kuvunja ndoa kwa ajili ya ila umo mikononi mwa mke peke yake wala si kwa mume kwa sababu mume anaweza kujiepusha na madhara ya mke kwa kumpa talaka (kumuacha) lakini mke hana uwezo huo ila uwezo wa kutaka kutengana."

Na wakakubaliana Shia, Malik, Shafi na Hambali kwamba: "Haki ya kuvunja ndoa imo mikononi mwa wote mume na mke itakapopatikaniwa ila, kwa sababu wote watadhurika na ila hizo zitakazopatikana, na uwezo wa kutoa talaka hauwezi kumkinga yeye na madhara ya ila hizo kwa sababu katika kutoa talaka kuna uwajibikaji wa kumsimamia mke kinyume na kuvunja ndoa kama nitakavyoeleza huko mbele.

Na yametofautiana madhehebu haya juu ya ila inayopelekea kwa uvunjaji wa ndoa.

**Vitu vinavyopelekea kuvunja ndoa**

Wanaelezea wanavyuoni wa Shia na madhehebu ya Sunni matatu (Malik, Hambali na Shafi) kuhusu ila zitakazopatikana kwa mwanamke hata mume akawa na haki ya kuvunja ndoa. Na kama zifuatavyo:

1. Uwendawazimu: Nao ni upungufu wa akili uwe ni wa masaa ama wa kudumu pasipo na kupotelewa na fahamu wala kupatwa na kifafa. Madhehbu yote hayo yamekubaliana kuwa ni haki kwa mume kuvunja ndoa atakapojuwa hilo baada ya ndoa.

Ama atakapokumbwa na maradhi haya ya wazimu baada ya ndoa na kabla kuingiliana basi wengi wamesema kuwa mume hafai kuvunja ndoa. Na mke atakapokumbwa na wazimu baada ya kuingiliwa basi wanavyuoni hawa wote wamekubaliana kuwa ndoa haipaswi kuvunjwa.

2. Ukoma: Nayo ni maradhi yanayokula nyama na kusababisha kuanguka kwa viungo vya mgonjwa na yanatia wasiwasi wa moyo. Na wakati mwengine huambukiza na kuenea kwa mwengine na hili wamelikubali madhehebu yote yaliyotajwa.

3. Mbalanga: Nayo ni maradhi maarufu hutokeza kama vitu vyeupe juu ya ngozi. Na hili pia umekubalika kati ya madhehebu kwa kuvunja ndoa.

4. Upofu: Nao ni kutoona hata kama macho yamefunguka wala usiwe ni uchongo wala maradhi ya kutoona usiku usiku peke yake (*nyctalopia*) wala maradhi ya upungufu wa nguvu za kuona pamoja na kumwaga machozi mengi (*bleariness*).

Atakapojua mume baada ya ndoa kwamba mkewe ni kipofu ana haki ya kuvunja ndoa kwa kukubaliana wanavyuoni wa Shia ama wanavyuoni wa Sunni hawaoni kwamba hiyo ni sababu.

5. Kiwete (kilema): Wanavyuoni wengi wa Shia

wameichukulia kuwa ni miongoni mwa sababu za kupelekea mtu kuvunja ndoa. Wakatofautiana kuwa jee ni yule kiwete asiyeweza kusimama kabisa (*incapacitated)* kama walivyosema wanavyuoni wa kale wa Shia, ama inaamanisha kiwete yeyote yule kama vile walivyoonelea wanavyuoni wengi wa wakati huu.

Ama madhehebu ya Sunni hawaoni hii kama ni moja ya sababu ya kuvunja ndoa.

6. Ila ya Kizazi (uzao): Ambayo inaleta pingamizi wakati wa kuingiliana na wakaelezea wanavyuoni wa Shia kuwa ni kuwepo kwa mfupa ama nyama 1. iliyozidi katika uzao, wakaeleza kuwa pia kushikana kwa uzao. Na wengi wakaongezea kuwa kushikana njia mbili katika uzao pia ni sababu.

Ama Sayyid Shirazy ameeleza kuwa ni ila yoyote ya kizazi: na inatakiwa hukumu iwe vile vile katika kila ila inayozuia kuingiliana, na ila zilizotangulia, na maneno haya yametiliwa mkazo na mapokezi ya Da'aaim kutoka kwa Ali (a.s.) kwamba amesema katika hadithi. "Hakika mke hurudishwa kutokana na ukoma, maradhi ya ngozi, wazimu ama ila ya uchi inayozuia kuingiliana."

Na Hambali vile vile wamesema kila kinachotia pingamizi ya kuingiliana au ladha na malengo ya kuingiliana basi linastahili kupelekea kuvunjwa kwa ndoa. Na hivyo hivyo wamesema Malik na Shafi.

## Hukmu za kuvunja ndoa

Hakika ndoa huvunjwa kwa ila ya mke iliyopatikaniwa kwake kabla ya ndoa na mume hakuijua mbeleni. Ama ila zinazotokea baada ya ndoa ima kabla ya kuingiliana ama baada yake, huwa hazichukuliwi kama sababu ya kuvunja ndoa.

Na kama inavyofaa kuvunja ndoa ya kuendelea kwa ajili ya ila hizi, pia katika ndoa ya muda (mut'a) wako baadhi ya Shia wanayosema hayo. Na lau mume ataridhika na ila hizo mapema basi hana haki ya kuvunja ndoa. Na pia atakapogundua ila hizi kwa mke lakini akanyamaza kwa mda pia hana haki tena ya kuvunja ndoa.

Na wakasema Hambali - Haki ya kuvunja ndoa haiondoki hata kama mume atachukuwa muda kuamua madamu hakuna kitu kinachoonesha kuwa ameridhika na ila zile au dalili kama vile kustarehe naye kimwili.Na anafaa mume kuvunja ndoa kufuatia moja ya ila zilizotangulia kwa mwanamke pasi na kutoka ruhusa kwa hakimu wa sheria. Haya ni kwa upande wa Shia. Ama kwa upande wa madhehebu ya Sunni wamesema ni lazima waende kwa kadhi ahukumu.

**Baina ya kuvunja ndoa na talaka**

Kuvunja kwa ndoa kunatafautiana na talaka kwa nukta zifuatazo:

1. Kuvunja ndoa hakuhitaji kutoa matamshi maalum kama vile katika talaka bali hutokea kwa kila kinachojulisha kuwa ndoa imevunjika.

2. Sio lazima kuwepo kwa mashahidi wawili waadilifu katika kuvunja ndoa bali ni sharti katika talaka kama ilivyo kwa Shia.

3. Kuvunja ndoa hakuhesabiwi kuwa miongoni mwa talaka tatu ambazo huwa ni haramu baada ya hapo kumuoa tena mwanamke mpaka aolewe na mume mwengine kisha aachwe. Atakapovunja ndoa kwa ajili ya ila kisha akamuowa tena halafu akamtaliki basi hiyo huhesabiwa kuwa ni ya kwanza na kule kuvunja ndoa hakuhesabiwi. Na hivi ndivyo wasemavyo Shia, Shafi na Hambali. Ama Hanafi na Malik wanahisabu kuwa kuvunja ndoa ni miongoni mwa talaka tatu.

4. Akimuacha mke kabla ya kumuingilia atampa nusu ya mahari. Ama akivunja ndoa kwa ajili ya ila basi mahari yote hurudishiwa mume na mke hana haki ya kupata chochote.

## MKE KUTAKA KUVUNJA NDOA

Yatakapokosekana maelewano na makubaliano kutoka pande zote mbili katika maisha ya mume na mke basi wote wawili watakuwa ni wenye kudhurika. Lakini mke ndiye atakuwa ni mwenye kudhurika zaidi kwa sababu mume ana uwezo wa kuvunja ndoa wakati wowote atakapo kupitia talaka ambayo Mwenyezi Mungu amempa uwezo wa kufanya hilo. Ama mke hana njia ya kujitoa ila kwa mipaka fulani michache.

Hivyo basi sheria imempa haki ya kuvunja ndoa iwapo atamkuta mume wake na baadhi za aibu za kimsingi kama vile ilivyompa mume nafasi hiyo iwapo atapata baadhi ya hitilafu kwa mke. Na iwapo katika baadhi ya maswala ya fiqh kwa kuna mambo yanayomlinda mke katika maudhui haya (ya kuvunja ndoa). Tutayaelezea katika uchambuzi.

Hanafi wameeleza kuwa kuvunja ndoa kwa sababu ya hitilafu ni kwa mke peke yake kwa sababu mume anaweza kujiepusha na madhara ya mke wakati wowote ule kupita talaka lakini mke hana uwezo wa kutoa talaka bali ana haki ya kutaka utengano ili kujiepusha na madhara ya mume iwapo atakuwa na ila.

Haifai kwa mume kuvunja ndoa zitakapotokeza baadhi ya ila kwa mke baada ya ndoa. Lakini mke anao uwezo huo zitakapojitokeza baadhi ya ila kwa mume hata kama ni baada ya ndoa na kuingiliana kama vile kutokuwa na uwezo wa kutoa mbegu za uzazi.

Na wakasema wanavyuoni wengi kuwa uwedawazimu (upungufu wa akili) kwa mume unamuwezesha mke kuvunja ndoa wakati wote utakapojitokeza.

Haya yote na mfano wake ni kwa ajili ya kumlinda mwanamke na maslahi yake.

**Mambo yanayopelekea kuvunja ndoa (upande wa mke)**

Wameelezea wanavyuoni wa kiislamu juu ya mapokezi mbali mbali kwamba inafaa kwa mwanamke kuvunja ndoa na mumewe baada ya kuolewa iwapo mume atakuwa na hitilafu ama moja ya ila zifuatazo.

1. Iwapo mume atakuwa amekatika uume wake na kutomuwezesha kumuingilia mke wake.

Wamekubaliana wanavyuoni wa kiislamu kuwa atakapojuwa mke baada ya ndoa kwamba mume wake hana kiungo cha uume basi ana hiari kwake kuvunja ndoa. Na lau kama tatizo hilo kwa mume litatokea baada ya ndoa wamesema wanavyuoni wa Sunni na wengi katika wanavyuoni wa Shia kwamba vile vile mke ana haki ya kuvunja ndoa.

Ama iwapo tatizo hilo litatokea baada ya kuingiliana Hanafi, Malik na Hambali wameeleza kwa njia mbili. Kwamba ila hiyo ikitokea baada ya kuingiliana basi mke hana hiari ya kuvunja ndoa.

Na Shafi na Hambali wakasema kwa njia nyengine kuwa ni hiari ya mke kuvunja ndoa ima ila hiyo itapatikana baada ya kuingiliana ama kabla.

Na wakahitalifiana wanavyuoni wa Shia kuhusu hiari ya mke kuvunja ndoa ila ikitokea baada ya kuingiliana. Wengi wamesema kuwa hana hiari, na wengine wakasema kuwa mke ana hiari ya kuvunja ndoa ima ila ikitokea kabla ama baada ya ndoa ama baada ya ndoa na kuingiliana.

2. Ukosefu wa nguvu za kiume (kutosimika) na kushindwa kufanya tendo la kuingiliana.

Na wamekubaliana wanavyuoni wa kiislamu kuwa hilo ni miongoni mwa ila zinazompa mke uwezo na haki ya kuvunja

ndoa atakapojuwa kuwa mume wake ana ila hiyo baada ya ndoa lakini iwapo atapendelea kukaa na mume wake kwa hali hiyo hiyo basi ndoa yao inafaa na hana hiari baada ya hapo ya kuvunja ndoa kwa maana alikuwa tayari amekubali kuishi nae kwa hali hiyo.

Na akiamua kuvunja ndoa basi jambo hilo liamuliwe na kadhi kisheria ambapo atatowa muda wa mwaka mmoja kamili iwapo ila itapoa na kuwa sawa basi mke hana haki ya kutaka utengano. Na hali ikibaki hivyo hivyo baada ya mwaka basi watatengana na wala sio lazima kurudi tena kwa kadhi, hili ni kwa wanavyuoni wa Shia. Na wanavyuoni wengi wa Sunni wamesema kuwa ni warudi kwa kadhi ili akaamuwe utengano huo.

**Kujua kabla ya ndoa**

Wamesema Hanafi, Malik, Hambali na Shia kwamba mke atakapoolewa na mume na hali ya kuwa anajua kwamba mume huyo hana nguvu za kuingiliana na akaridhika basi hafai kulalamika mbeleni wala hana haki ya kuvunja ndoa. Ni sawa sawa na mnunuzi anapojua kwamba bidhaa ina hitilafu kisha akaridhika na kuinunua basi huwa ameikubali bidhaa ile.

Lakini Shafi wakasema kuwa atakapojua mwanamke kuwa mwanamume ana matatizo ya nguvu za kiume kisha akakubali aolewe naye hivyo hivyo, basi haki yake ya kutaka kuvunja ndoa hubaki pale pale kwa sababu atakuwa amekubali.

**Kupoteza nguvu za kiume baada ya kuingiliana**

Atakapomuingilia mume mke wake japo mara moja kisha akapoteza nguvu za kiume basi mke hana haki ya kutaka kuvunja ndoa ama utengano. Haya ni kwa mujibu wa wanavyuoni wengi wa Sunni.

Na wakakubaliana wanavyuoni wa Shia kwamba mke ana

hiari ya kutaka utengano iwapo mume wake atapoteza nguvu zake za kiume ima kabla ama baada ya ndoa. Ama mume akipoteza nguvu zake za kiume baada ya kumuingila mkewe hata kama ni mara moja basi wametofautiana kuwa jee mke anakuwa na hiari ya kuvunja ndoa ama la.

Amenukuu mwenye *Jawaahir* kutoka kwa Ibni Zuhra na Sheikh Mufid kuwa mke anao uwezo wa kutaka utengano ama kuvunja ndoa. Na akapokewa Kinaaniyyu kuwa amesema: "Nilimuuliza Imam Sadiq (a.s.) juu ya mke ambaye mume wake amekumbwa na mtihani kwa njia ambayo hawezi kutenda tendo la kuingiliana kimwli kabisa, jee atenganishwe? Akasema Imam, ndiyo, iwapo atataka hivyo mke. Na mapokezi mengine mengi ijapo juu ya hilo. Na amelemea katika maoni haya Sayyid Shirazy katika wanavyuoni wa leo."

Amesema katika (Al-Fiqh) na hata tusiposema kuwa mke ana haki ya kutaka kuvunja ndoa, ni juu ya kadhi kuamrisha kutolewa talaka kwa ajili ya kuwa ni wazi kwamba mwanamke anahitaji mwanamume, kuishi bila ya kuingiliwa ni jambo zito kwa wanawake wengi na kuleta madhara ya kiafya wakati mwengine. Na uwazi ni kuwa ukosefu wa nguvu za kiume pia mtu anapopooza viungo vyake kwa njia ambayo hawawezi kutenda kitendo cha kuingiliana.

3. Maksai (*Castration*) nayo ni kuvunjwa kordani mbili ya mwanamume na kumfanya asiwe na nguvu za kufanya tendo la ndoa. Na Hanafi wakasema kuwa mke ana haki ya kutaka utengano na mume wake baada ya mume kupewa muda wa mwaka mmoja kamili na kadhi. Na Malik wakasema ni juu ya mke kuamua iwapo mume hawezi kutoa manii. Na Shafi wakaeleza kwa njia mbili kuwa mke anaweza kutaka utengano na njia nyengine kuwa mke hawezi kutaka utengano. Na Hambali wakasema kuwa mke hawezi kutaka utengano maadamu mume anazo nguvu za kuingiliana.

Na wakaonelea wanavyuoni wengi wa Shia kuwa mke anayo haki ya kutenga na akaitilia shaka Sayyid Sistaaniy.

4. Upungufu wa akili, ukoma na mbalanga.

Hanafi hawaonelei kuwa ni ila zimpelekezo mke kutaka utengano, iwe ni kwa mke ama mume. Na madhehebu mengine yaliyobaki yamesema kuwa mume anayo haki ya kutaka utengano iwapo mke atakumbwa na maradhi ya upungufu wa akili, ama akiwa mume ndie mwenye kukumbwa basi pia mke ana haki ya kutaka utengano. Na wakasema Malik, Shafi na Hambali kuwa mke anayo haki yakutaka utengano lakini ama Shia baadhi ya wanavyuoni wao wamesema kuwa maradhi ya akili kwa mume humpa mke uwezo wa kutaka utengano, yawe yatakuwa ni maradhi ya kudumu ama ya muda kwa muda iwe itakuwa baada ya ndoa ama baada ya kuingiliana hata kama wana watoto kiasi gani.

Na wakasema tofauti na hayo kwa mwenye ukoma na maradhi ya mbalanga ambapo baadhi yao wamesema kuwa mke hana haki ya kutaka utengano kwa sababu ya maradhi haya mawili, lakini kuna baadhi ya wanavyuoni wa kale na wengine wa leo ambao wamesema kuwa mke ana haki ya kutaka utengano iwapo mume ataugua maradhi haya kwa sababu huenda akadhurika na kuambukizwa kama alivyosema (a.s.): "Mkimbieni mwenye ukoma kama mkimbiavyo simba." Na lengo la kukimbia hapa ni kwa ajili ya kuambukizwa. Kulingana na hayo inaonyesha kwamba mke ana uwezo wa kutaka utengano ingawa wengi wamesema kuwa hana haki.

**Udanganyifu na kuvunja ndoa**

Kutangamana na watu ni lazima kuwe na ukweli na uwazi ili mafungamano yawe imara na ya kuendelea kwa ajili hiyo yamesisitiza mafunzo ya kiislamu juu ya ukweli na uwazi juu

ya pande zote mbili zinapotangamana, ili kila upande ujuwe unachukua nini na kutoa nini, wala kusiwe na udanganyifu. Hivyo basi sheria imeharamisha kila sampuli ya udanganyifu.

Amesema (s.a.w.) "Si sawa kwa Musilamu atakapo muuzia ndugu yake bidhaa yenye hitilafu na asimjulishe mapema."

Na akasema tena (s.a.w.) "Si miongoni mwetu (Waislamu) mwenye kumdanganya Muislamu katika bidhaa."

Na ikapokewa kwa Imam Ali (a.s.): "Mtu muovu ni yule mwenye kudanganya watu kwenye bidhaa."

Na kwa kuwa mafungamano ya mume na mke ndiyo ya juu na muhimu miongoni mwa mafungamano, basi yanatakiwa yawe juu ya misingi ya ukweli na uwazi ili yasikumbe na misukosuko na kuvunjika.

Na kwa ajili hiyo yametilia mkazo mafunzo ya Islamu umuhimu wa kujichagulia kwa pande zote mbili na pia kufaidika na maoni ya watu wema kabla ya kuchagua na kukubali na pia vile vile kutowa nafasi ya kujuana na kujuwa utu wa mwengine.

Na ikatenga Sheria jambo hili kuwa si miongoni mwa Ghiba (kumtaja mtu kwa asilolipenda) ambalo ni haramu kisheria kwani pale mtu anapotaka ushauri kwa mwengine juu ya kuchaguwa mke au mume basi hapana budi mtu aelezwe uhakika ulivyo hata kama kutakuwa na mambo ya aibu juu ya yule auliziwaye basi hapana dhambi wala makosa kulingana na sheria ijapokuwa hilo limo katika maudhui ya ghiba kwa sababu ghiba ni kumtaja nduguyo kwa achukialo na kudhihirisha aibu zake. Lakini kulingana na hili limevuliwa kutoka sehemu ya ghiba.

Na si sawa kwa mmoja kati ya pande mbili (mume au mke) kuficha aibu aliyonayo au kujisifu kwa kitu asicho nacho. Basi kutakapokuwa na hitilafu kwa mke ama mume na kuificha mpaka ndoa ikapita basi hapo kutakuwa kumedhihiri udanganyifu na hiana.

Vile vile lau mmoja atajisifu kwa sifa asiyokuwa nayo kama vile utukufu, nasaba, uzuri na kuwa ni bikra na mfano wa hayo na ndoa ikapitishwa kwa ajili ya kupendezewa na sifa hizo basi huo ni udanganyifu.

**Namna za udanganyifu**

"*Tadlis*" ni kudanganya kwa kuficha aibu iliyopo na kudai ukamilifu usiopo. Na mara nyingi "*Tadlis*" hutumika kwa udanganyifu wa sifa za binaadamu. Na "*Ghish* hutumika katika udanganyifu wa sifa za bidhaa.

Na udanganyifu ambao unapelekea kuwepo kwa haki ya kutaka kuvunja ndoa ni kwa namna tatu:

1. Atakapopelekewa mtu kuoa kwa ajili ya sifa alizosifiwa juu ya mke ama mume kisha ikadhihiri kuwa sifa hizo hazipo, basi mume ama mke ana haki ya kuvunja ndoa kama vile mume akiambiwa kuwa mke ni bikra, ama hana maradhi fulani, ama mwenye sifa fulani kisha ikadhihiri kinyume cha hayo basi ana haki ya kuvunja ndoa.

   Vile vile lau atajulishwa kuwa mume ni katika familia fulani, au mwenye cheo fulani au ni mzima hana maradhi fulani ni jambo hilo likampelekea yeye kuolewa na mume huyo, kisha akagundua kuwa mambo ni kinyume na alivyosifiwa basi pia yeye ana haki ya kuvunja ndoa.

2. Ni kutajwa sifa hizo wakati wa ndoa kama kumsifu mmoja (mume ama mke) kama kusemwa 'Nimekuoza mke huyu bikra au asiye mke mkuu, au aisyekuwa na maradhi au mwenye sifa fulani.' Au kusemwa kwa niaba ya mume kuwa nimekuozesha mume huyu wa kabila la Hashimiya ama mwanachuoni na mfano wa hayo kisha ikabaini kutokuwepo kwa sifa hizo zilizotajwa wakati wa ndoa basi huo ni udanganyifu (*Tadlis*) humpa mtu haki ya kuvunja ndoa.

3 Ni kuwa yakamilike mazungumzo na makubaliano kati ya pande mbili au kwa mwenye kuwakilisha kuwa kuna sifa fulani zilizopeleka ndoa basi hapa hata kama hazitotajwa sifa hizo wakati wa kufunga ndoa na ikabaini baadaye kuwa ni kinyume cha hivyo basi haki ya kuvunja ndoa ipo.

Basi kwa mambo matatu kama huyu huwa udanganyifu umedhihiri na hupelekea kuwepo kwa haki ya kuvunja ndoa. Lakini iwapo hakutotajwa sifa zozote za kumhusu mume au mke katika ndoa na yasitimu makubaliano juu ya sifa hizo, lakini mmoja awe anatarajia kupata sifa hizo kwa mwengine au anadhania kuwa sifa hizo zipo na kumpelekea yeye kufunga ndoa, kisha baadaye ajuwe kuwa sifa hizo hazipo kwa mume ama mke basi hapo hapana haki ya kutaka kuvunja ndoa kwa sababu dhana hiyo yake haikuwa ni yenye kutajwa mbele ya mwengine, basi hali kama hii haipo katika mambo yale matatu yaliyotajwa hapo mbeleni, hivyo basi hapana haki ya kutaka kuvunja ndoa.

Kwa mfano asitajiwe mume kuwa mke ni bikra na hilo pia lisitajwe kama sifa ya mke wakati wa ndoa na kusipite mazungumzo yoyote juu ya hilo mda mchache kabla ya ndoa, na mume anatarajia tu na kudhania kuwa mke ni bikra kisha akute mambo kinyume cha hayo basi mume hana haki ya kutaka kuvunja ndoa. Na wala jambo hilo ni wajibu kwa watu wa mke au mke mwenyewe kumueleza mume juu ya hilo.

Lakini jambo kama hilo mume aweza kulichukulia kwa njia hino: Atake tofauti ya mahari ya bikra na asiye bikra, iwapo kwa mfano mahari ya bikra ni elfu ishirini (20,000) na ya asiye bikra ni elfu kumi na tano (15,000) na tayari alikuwa ashatowa elfu ishrini (20,000) basi ni haki arudishiwe elfu tano (5,000)

**Kuchukua hatua ya kuvunja ndoa**

Wakati itakapobaini kwa mume ama mke kwamba zile sifa hazipo kulingana na mambo yale matatu yaliyotajwa hapo mbeleni basi atakuwa na hiari yakuvunja ama kuendelea na ndoa kwa kuhalifu shart waliyokubaliana, basi hapana budi ya kuchukuwa hatuwa ya kuvunja ndoa akitaka.

## MAONI YA MADHEHEBU YA SUNNI

Limesema dhehebu la Hanafi kwamba atakapopendelea mmoja kufunga ndoa kwa ajili ya sifa ya mwengine (mume ama mke) aliyapenda na ikawa ni kinyume cha hivyo, basi hana hiari ya kuvunja ndoa.

Na iwapo atatozwa mahari zaidi kwa ajili ya sifa hiyo, kama vile kuwa bikra na isiwe hivyo basi haitomlazimu yeye kutoa ziada ya mahari.

Amesema Sheikh Muhammad bin Abdul Wahid maarufu anajulikana kama Ibnul Hammam katika kitabu chake (Fat-hul Qadir) na katika ndoa lau atapelekwa mtu kuowa kwa sifa alizozipenda kama vile bikra, uzuri, umbile na umri mdogo, na kumbe mke akawa si bikra, ni mkubwa kiumri mwenye umbile lisilovutia, mwenye kutokwa na nyute, na akili pungufu basi hana hiari ya kuvunja ndoa kwa hayo.

Na Malik wameonelea kuwa mtu ana hiari ya kuvunja ndoa wakati mambo yatakuwa kinyume na sifa alizosifiwa na hivyo hivyo wamesema Shafi.

Na wakatenganisha Hambali baina ya kusifiwa mtu kwa sifa yakuwa huru, au ni katika familia tukufu kisha idhihiri kuwa yeye ni mtumwa au katika kabila duni, basi hapo mtu ana hiari ya kuvunja ndoa. Ama zitakapokuwa sifa hizo hazilingani na "*Kafaa*", kama vile mjuzi au mzuri akipata kinyume cha hayo basi hana hiari ya kuvunja ndoa.

Na vile vile lau itampelekea mtu kuowa mke kwa kuambiwa kuwa ni muislamu kisha ikambainikia kuwa si Muislamu basiatakuwa na hiari ya kuvunja ndoa. Ama atakapoelezewa kuwa ni bikra kisha ikabainika kuwa si bikra basi Ahmad Bin Hambali amesema kauli mbili: Kuwa mume hana hiari ya kuvunja ndoa, na nyengine kuwa anayo hiari.

## USIKU WA MAHARUSI NA KUINGILIANA

Usiku wa maharusi ndivyo chanzo cha kuanzisha maisha ya bibi na bwana kupitishwa kwa ndoa ni chanzo cha kuanzisha mafungamano kati ya mke na mume na huwa wamekuwa kama bibi na bwana kisheria. Lakini kwa "*Zafaaf*" usiku wa maharusi kunaingia makubaliano ya kimume na mke kivitendo ambapo wao wawili huanza kuishi kivyao wakishirikiana kimaisha na makaazi na kusaidiana kimaisha.

Kwa kupitia usiku wa maharusi mume na mke huwa wanayaaga maisha ya upweke na ukapera na kuanzisha familia yao na kizazi kipya.

Na maana ya "*Zafaaf*" kilugha ni mke kutulia kwa mume wake.

Imekita katika mawazo ya watu katika jamii yetu kuwa kuna nyusiku ambazo watu wanafaa kujiepusha na kufanya harusi.

Na tumetafiti katika maudhui (mapendekezo na machukizo ya ndoa) eti imepokewa kuwa kuna nyakati ambazo ni machukizo kupitisha ndoa hasa iwapo kamari katika buruji ya nge, na hili linaendelea kwa muda wa siku mbili na robo, yaani usiku miwili au mitatu, ambayo inatofautiana na mwezi mwengine. Haya ni kwa kutegemea mapokezi ya Imam Jafar Sadiq (a.s.) "Mwenye kumuoa mke na Q*amari* (mwezi) upo katika buruji ya nge basi hajaona uzuri."

Na hapo ndipo walipoweka mpaka wanvyuoni wengi wetu waliotangulia, ambapo hawakueleza machukizo ya kufunga ndoa nyakati nyengine.

Nao ni kama Sheikh As-Saduk, Mufid, Tusi, Muhakkikul-Hulliy, Shahidain, mwenye Jawahiri na wengineo.

Lakini baadhi ya wanavyuoni wa hivi punde wameongezeamachukizo ya kupitisha ndoa kamari itakapokuwa mwisho wa mwezi, unapokuwa mchanga muangaza wa mwezi wa muandamo usiku wa tarehe 30, 29, 28.

Ambapo kumepokewa mapokezi Mursal kwamba "imechukizwa kuoa mwisho mwisho wa mwezi: Na mapokezi mengine kutoka kwa Al- Imam Al-Hadi (a.s.).

Kisha wakaongeza wanavyuoni wengi machukizo ya kufunga ndoa katika siku saba za mwezi (3, 5, 13, 16, 21, 24, 25) kwa kuwepo mapokezi yanayosema kuwa hizo ni siku za visirani lakini hakupatikana mapokezi yaoneshayo machukizo ya usiku wa maharusi katika siku hizo.

Mukabala ya hayo kuna mapokezi yanayomuelekeza mwanaadamu kumtegemea Mwenyezi Mungu na kujikinga kwa dua na Aya za Qur'an, kutoa sadaka na kutotilia umuhimu juu ya visirani kwa baadhi ya masiku. Na yale waliyoyataja wanavyuoni ni katika kupitisha ndoa. Lakini *Zafaaf* na usiku wa kuingiliana hawakutaja machukizo yafikapo katika nyakati hizo.

Na kwa ajili hiyo hapana haja ya mtu kujiepusha na nyusiku hizo anapochagua usiku wa maharusi (wa kuingiliana).

## CHAKULA CHA HARUSI (*WALIMA*)

Imependekezwa kulisha wakati wa harusi. Imepokewa kutoka kwa Ali Ar-Ridha (a.s.) kuwa Mtume (s.a.w.) amesema "Hakika katika Sunna za Mitume ni kulisha watu wakati wa harusi."

Na akapokea Ahmad katika Hadithi ya Buraydah amesema: "Alipomposa Ali Fatma alisema Mtume (s.a.w.) kuwa hapana budi wakati wa harusi kuwe na chakula."

Na Mtume (s.a.w.) alimwambia Abdulrahman bin Auf alipokuwa anaoa: "Lisha chakula hata kama ni kwa (kuchinja) mbuzi mmoja."

Basi chakula wakati wa harusi ni Sunna iliyopendekezwa na wanavyuoni wote na ni mashuhuri katika dhehebu la Malik na Hambali na maoni ya baadhi ya Shafi, na pia katika maneno ya Malik na dalili ipo katika kitabu cha Shafi *Al-Ummu.*

Na maoni ya Dhahiriyah ni kwamba chakula cha harusi ni lazima, kulingana na maneno ya Mtume (s.a.w.) kumwambia Abdulrahaman bin Auf, "lisha chakula hata kama ni kwa (kuchinja) mbuzi mmoja."

Ni kuitikia mwito wa chakula cha harusi ni jambo lililopendekezwa kulingana na dhehebu la Shia.

Ama wanavyuoni wengi wa Sunni wamesema kuwa kuitikia mwito wa chakula cha harusi ni jambo la lazima, kulingana na Malik, Shafi na Hambali ambapo hapana kutoa udhuru kwa ajili ya kuwepo baridi, joto ama shughuli, kulingana na Hadith:

"Na anaealikwa katika chakula cha harusi na asihudhurie basi hakika amemuasi Abal Qasim."

Na jambo la kukumbushana ni kuwa namna mambo yanavyotendeka katika chakula cha harusi, mahali ambapo pengi hufanyika israfu na mtu kujifakhirisha kwa chakula hicho. Na pia namna ya uandazi wa chakula katika harusi zetu

bado upo katika namna ya kale, ambapo sahani za vyakula huandaliwa na kujazwa na kuliwa na watu kidogo, watu hula kidogo kisha huacha na chakula humwagwa. Na nimesikia kutoka pande nyingi katika jamii yetu ambapo thuluthi ama nusu ya chakula hubaki na kumwagwa baharini ama jaani.

Je iwapo hii sio israfu (uharibifu) basi israfu na uharibifu ni upi?

Anasema Mwenyezi Mungu (S.W.T.) katika Suratul Israa :27: "Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu wa mashetani."
Na akasema katika Suratul Aa'raf : 31: "Kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri) lakini msipite kiasi tu. Hakika Yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao kiasi."

**Sherehe za usiku ya maharusi "*Zafaaf*"**

Hudhihirisha jamii za maharusi wawili na marafiki zao furaha na bashaha usiku wa mahrusi kulingana na sherehe walizozowea kila jamii kwa namna yake. Na pia maharusi hujitahidi kudhihirisha uzuri wao na mapambo yao hasa kwa mwanamke.

Amesema mmoja wa watafiti wa mambo ya kijamii: "Siku ya maharusi ni siku pekee ambayo macho yote huwaangalia maharusi hao peke yao, kwa ajili hujitahidi awe mzuri zaidi katika siku hii (mke) kuliko masiku yote ya maisha yake. Ni sababu pekee inayomfanya kila mwanamke ahisi kwamba siku ya harusi yake ndiyo siku nzuri na bora katika maisha yake na kumfanya aikumbuke maishani mwake yote. Ni huwa ni kama ambaye hajaona uzuri wa hakika kabla ya siku hiyo ama baada ya hiyo. Hili si kwa sababu ati ndoto yake nzuri aliyokuwa akitarajia kwa muda mrefu imekuwa kweli, ama kwa sababu amekuwa mwenye kumiliki nyumba, la! Bali ni kwa sababu alikuwa amepambwa na akawa mzuri sana kuliko siku nyengine yote ya maisha yake, kabla na baada ya kuolewa.

Na kwa sababu yeye pengine kwa mara ya kwanza alikuw

ndiye mzuri kuliko watu wote waliohudhuria, na ni yeye pekee ambae macho yote yanamuangalia. Basi uzuri wowote na furaha katika fikra ya mwanamke haushindii huu wa siku ya harusi.

Basi ikiwa ni katika desturi kuwepo sherehe za kusherehekea usiku wa maharusi, sherehe za kusherehekea usiku wa maharusi, basi mafunzo ya dini pia yameshajiisha juu ya hilo.

Lakini baadhi ya jamii hupita mipaka katika kufanya sherehe hizi na kutumia mali nyingi kupita kiasi na kujikalifisha.

Mahitaji ya harusi hutumika kwa namna tatu:

1 Mahari

2 Vyombo vya nyumbani

3 Matumizi machache ya kutumika wakati wa sherehe ya usiku wa maharusi.

Na mara nyingi hili la tatu huwa ni lenye gharama nyingi kuliko yale mawili ya mwanzo, kwa sababu mahari na vyombo vya nyumbani hubaki na maharusi hufaidika nayo. Lakini hawafaidiki na yale yanayotolewa kwa wengi kwa ajili ya sherehe ili hubaki utajo tu na ufahari. Na mfano wa haya ni mengi kama vile kumbi za ufahari, kukata keki, vyakula vya hali ya juu na kadhalika.

**Yaliyopendekezwa siku ya maharusi**

Wametaja wanavyuoni baadhi ya yaliyopendekezwa anapomuingilia mume mkewe usiku wa maharusi miongoni mwayo! Udhu: Wote wawili watawadhe na kuswali rakaa mbili kujikaribisha na Mwenyezi Mungu. Na kila mmoja alete utajo wa Mungu kwa kumshukuru na kumsalia Mtume na familia yake na kuomba mapenzi, upole na uwezo wa kuendesha maisha yao. Na katika dua zilizopokewa ni kusema:

LLAHUMMA RZUQNIY ULFATAHAA, WA WUDDAHAA WA RIDWAA HAA BIY ARDHWINIY BIHAA, WA AHSIN BAINANAA BIAHSANI IJTIMAAI, WA ANFASA I'TILAAF, FA INNAK ATUHIBBUL HALAALA, WA TAKRAHUL HARAAMA

Yaani: Ewe Mola nipe mapenzi yake, upole wake na aridhike na mimi na uniridhishe naye na utupe mafungamano bora.

Hakika yako wewe unapenda yaliyoruhusiwa na kuchukia yaliyokatazwa. Na hii ni dua ambayo Muhammad Al-Baqir (a.s.) alimfunza mmoja wa jamaa zake.

Na pia mume aweke mkono wake wa kulia juu ya kichwa cha mke wake huku ameelekea kibla na amuombe Mwenyezi Mungu baraka na uwezo wake na aombe dua iliyopokewa kutoka kwa Imam Jafar As-Sadiq (a.s.)

ALLHUMMA ALAA KITAABIKA TAZA WWAJTUHAA, WA FIY AMAANATIKA AKHADHTUHAA, WABIKALIMAATIKA ISTAHLALTU FARJAHAA, FAINA KADHWAYTU FIY RAHIMIHAA SHAIAN FAJ-ALHU MUSLIMAN SAWIYYAN, WALAA TAJ-ALUHU SHIRKA SH-SHAITAAN

Yani: Ewe Mola wangu nimemuoa kwa njia yako, na nimemchukua kwa amana yako, na kwa maneno yako imekuwa halali kwangu tupu yake basi nikitia kitu katika uzao wake basi kifanye kiwe ni mtoto Muislamu wa kweli, wala usikifanye kuwa kiumbe kitakachomfuata shetani.

Na nimepatikana katika vitabu vya Ahli Sunna kutoka kwa Abi Said bwana wa Abi Asyad kuwa Abdallah bin Masud na Aba Dharri na Hudheifa na wengineo miongoni mwa sahaba za Mtume (s.a.w.) kuwa walimwambia: "Utakapoingia kwa mkeo, swali rakaa mbili, kisha umshike kichwa chake na useme: "ALLAHUMMA BAARIK LIY FIY AHLIY, WA BAARIK LIAHLIY FIYAA, WARZUQHUM MINNY WARZUQNIY MIN-HIM

Yaani: Ewe Mola wangu ibariki familia yangu na unibariki mimi kupitia wao, na uwaruzuku kupitia mimi na uniruzuku mimi kupitia wao.

Na akapokea Abu Daud kutoka kwa Mtume (s.a.w.) dua ifuatayo:

ALLAHUMMA INNIY AS-ALUKA KHAIRAHAA, WA KHAIRA MA JUBILAT ALEIHI WA AUUDHUBIKA MIN SHARRIHAA, WA MIN SHARRIMA YUBILAT ALEIHI

(Ewe Mola wangu nakuomba uzuri wa mke huyu na uzuri uliopambiwa. Na najikinga kwa ubaya wake na ubaya uliopambiwa.)

Na ni wazi kwamba mapendekezo haya humfanya mume na mke kwanza maisha yao kwa mfumo wa dini na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Na pia huwa na matumaini ya moyo na kuwafanya wao ni wenye kufanikiwa na baraka, wema na mafanikio kutoka kwa Mwenyezi Mungu (S.W.T.).

**Kusherehekea harusi**

Ni katika desturi wakati wa harusi kuwepo shughuli ziletazo furaha kwa maharusi wawili, jamaa na marafiki. Na hilo linapelekea kuwepo kwa sherehe ili jamii idhihirishe furaha zake.

Na pia vile vile Uislamu umeruhusu sherehe kwa jili ya harusi kama ilivyopokewa katika baadhi ya Hadithi na mapokezi wengine na pia katika sera ya Mtume (s.a.w.). Na mfano mmoja tu unatutosha uliopo katika vitabu vya historia juu ya sherehe ya Fatima Az-zahra (a.s.) alipoolewa na Imam Ali bin Abi Talib (a.s.) sherehe ya bashasha iliyosimamiwa na Mtume (s.a.w.).

Na imepokewa na Dkt. Sheikh Muhammad Abdu Yamaaniy kwa njia ya Muhtasan juu ya sherehe hiyo katika kitabu chake (huyo ni Fatimah Az-zahra)

Ulifika wakati wa maharusi uliokuwa ukisubiriwa, na hakika

wameshereheka familia ya Abdul Muttalib harusi hii alikuja Hamza (r.a.) ami yake Mtume (s.a.w.) na ami yake Ali (Mungu autukuze uso wake) na ngamia wawili akawachinja na kulisha watu.

Na chakula hicho kilikuwa bora zaidi ya vyakula vyengine vya harusi, kwani ilikuwa ni harusi ya kwanza katika vijana na ya bintiye Mustafa (s.a.w.).

Na watu walipomaliza kula Mtume (s.a.w.) alitandika nguo juu yake kisha akamwambia Fatima, panda, na akamwambia Salman amuongoze njia na Mtume (s.a.w.) akawa anatembea nyuma yake pamoja na Hamza na Banu Hashim wakiwa wamenyanyuwa panga zao kisha akawaambia wanawake wa Abdul-Muttalib na wa Muhajirina na Ansaar wajiunge katika kumshindikiza Fatima (r.a.) na wafurahi washerehekee wapige takbira na washukuru Mwenyezi Mungu kwa kumsabihi na kuwa wasiseme ila yanayo mridhisha Mwenyezi Mungu.

Na Ummu Salama akawa anaimba mashairi na wanawake wengine wakiitikia kibwagizo na kupiga takbira.

**Nyimbo wakati wa harusi**

Wametofautiana wanavyuoni wa madhehebu ya Sunni juu ya hukumu ya kuimba. Wengi kati yao wakaeleza kuwa kusikiliza nyimbo inakuwa ni makosa na haramu zitakapoambatana na maovu, na kuhofiwa kupelekea kwa maovu ama iwapo zitapelekea watu kukosa kutenda wajibu mmoja miongoni mwa wajibu. Ama zikiwa nyimbo mbali na hayo zikawa ni kwa malengo ya kujifurahisha nyoyo basi hapo pana kutofautiana, baadhi yao wamesema yafaa na wengine wakapinga hilo.

Hanafi na baadhi ya Hambali wamesema kuwa ni makosa kwa dalili ya Qur'an

Luqman 6

“Na katika watu wako, wanaochagua maneno ya upuzi ili wapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu.”

Amesema Ibnu Abbas na Ibnu Masud kuwa maneno ya upuzi (*Lahwal hadith*) hapa kuwa ni nyimbo. Na kwa hadithi iliyopokewa na Abi Umamah (r.a.) kwamba Mtume (s.a.w.) amekataza kuuza vifaa vya nyimbo, na kuvinunua na kuchumia na kula faida yake.

Na Shafi, Malik na baadhi ya Hambali wakasema kuwa hilo ni makruh.

Na wakasema baadhi ya Hambali kama vile Abubakar Khallal na Abubakar Abdul-Aziz na miongoni mwa Shafi ni Ghazali kuwa hilo linafaa.

Ama wanavyuoni wa Shia wote wamesema kuwa ni makosa na haifai kulingana na hadithi za Maimamu wa Ahli bait (a.s.) katika kufasiri neno la Mwenyezi Mungu. Katika Suratul Hajj: 30

“Na jiepusheni na usemi na uwongo” kuwa maana yake ni nyimbo. Na pia katika kufasiri neno la Mwenyezi Mungu

Katika Suratul Luqman: 6

“Na katika watu wako wanaochagua maneno ya upuzi ili wapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu,” kwamba maana yake ni nyimbo.

Na pia katika Suratul Furqan: 72

“Na wale ambao hawashuhudii shahada za uongo,” kwamba ni nyimbo na wanapopita penye upuzi, hupita kwa heshima (yao). Aya hiyo hiyo kuwa wao wameacha kusikiza nyimbo, na ziko Hadithi nyingi juu ya hilo.

Haya ni kwa hukumu ya nyimbo kwa jumla.

Ama nyimbo katika harusi wamesema wengi katika wanavyuoni wa Sunni kwamba inafaa.

Na yaliyoruhusiwa na Uislamu na kupendekezwa ni nyimbo wakati wa harusi kufurahisha nyoyo na zinapaswa ziwe mbali na mambo ya ukosefu wa adabu, zisizo na tabia na maneno machafu.

Imepokewa kutoka kwa Amir bin bin Sa'ad (r.a.) amesema: :Niliingia kwa Qardha bin Ka'ab na Abi Masud Ansary wakiwa katika harusi pakawa pana watu wanaimba, nikawauliza nyinyi ni sahaba za Mtume wa Mwenyezi Mungu, na katika watu waliopigana vita vya Badr hawa wanafanya hivi mbele yenu! Wakasema: "Ukitaka kaa usikilize nasi na ukitaka waweza kwenda zako. Hakika tumeruhusiwa nyimbo wakati wa harusi." hadithi hii imepokewa na Nasaai na Hakim.

Na alisherehekea Bibi Aisha (r.a.) harusi ya Fariah binti As'ad na akampeleka hadi nyumbani kwa mumewe, Nabii bin Jabir Ansaary Mtume (s.a.w.) akamuuliza Aisha (r.a.): "Ewe Aisha hamukuwa na nyimbo? Kwani Ansaar wanapendezwa sana na nyimbo." Hadithi hii imepokewa na Bukhari, Ahmad na wengineo.

Na katika mapokezi mengine ya Hadithi hii kwamba Mtume (s.a.w.) alisema kumuuliza Aisha "Je mulimpelekea pamoja naye kijakazi akipiga tari na kuimba?"

Lakini wengi kati ya wanavyuoni wa Shia wamevua umakosa wa nyimbo katika harusi kwa wanawake peke yake, kwa masharti ya kuwa kusiambatane na chochote kilichoharamishwa, kama vile kusikiwa na wanaume wa kando ama kutumia vyombo vya mizuki, lakini baadhi ya wanavyuoni wake wakasema kwamba nyimbo wakati wa harusi ni makosa moja kwa moja.

**Wanaosema kwamba yafaa**

maoni ya wengi ya wanavyuoni wa Shia, amesema Sheikh Ansaary katika *Makasib*: "Nyumba wakati wa harusi zikiwa hazitoambatana na mambo yaliyokatazwa kama vile mambo ya upuuzi kutumia vifaa vilivyoharamishwa na wanaume kuingia kwa wanawake na kauli iliyo na nguvu ni hii ya kuvuliwa uharamu wake kwa wanawake."

Amesema Abu Busair kuwa nilimuuliza babake Abdallah As-Sadiq (a.s.) kuhusu pesa zipatikanazo kwa kuimba. Akasema: "Ni haramu kwa zile ambazo waume pia huingia lakini zinazopatikana kwa ajili ya harusi hazina makosa." Na ikiwa pato limeruhusiwa basi pia vile vile kitendo.

Na pia vile vile amesema kuwa yafaa mwenye *Al-Jawaahir* na Sheikh Yusuf Al-Bahraniy katika *Al-Hadaiq*.

Na katika wanaosema kwamba nyimbo zinafaa wakati wa harusi miongoni mwa wanavyuoni wa sasa ni Sayyid Muhammad Shirazy. Na wanaosema kuwa nyimbo zinafaa wakati wa harusi hata kama ni kwa kaseti ama kifaa chochote kama vile radio madam hayatashikamana na haramu ama makatazo mengine na pia kufaa kucheza wanawake wao kwa wao na kufaa kwa nyimbo katika harusi sio kwa usiku wa maharusi peke yake bali masiku yote ya harusi.

Na miongoni mwa wanaounga hilo ni Sabzuwary, Ruhaniy, Khamenei, na Sheikh Muhammad Amin Zeinuddin. Na kuonelea kuwa hapana makosa kwa wanawake kuimba na kutumia vyombo vya muziki wakati wa harusi.

Lakini wanavyuoni wengine akiwemo Sayyid Sistaaniy ametilia shaka hilo la kuruhisiwa wanawake kuimba wakati wa harusi na kuonelea kuwa hilo ni makosa hata wakati wa usiku wa maharusi.

**Kuweka kizuizi (Hijab) na kujikinga na maovu**

Katika sherehe nyingi za harusi mara nyingi watu huchukulia mambo urahisi katika kuchunga mipaka ya dini, hasa wanawake wanaohusika na harusi huwa wanajipamba kwa

hali ya juu kabisa na kutangamana na wanaume wanaohusika na harusi basi kwa hakika mahali kama hapa ni lazima pawe ni kizuizi cha kuwaziba wanawake ili wasionane na waume na kudhihirisha mapambo yao.

Na pia wanaume wanahitajiwa wayaepushe macho yao na kuwaangalia wanawake na kujitenga na sehemu zao. Na pia pasiwe na mchanganyiko kati ya waume na wake. Na sasa kumezuka mambo ya kupambwa bibi harusi katika ukumbi na kisha huingia na kaka zake na baadhi ya wanaume wengine na kutangamana na wanawake mambo yanayokhalifu sharia na yasiyokuwa na heshima bali wanahitajika wanawake wakae kwa hali ya heshima na kujisitiri ipasavyo jambo ambalo ni zito sana kwao wao hasa wakati wa sherehe kama hizi.

Na jambo jengine lililo kinyume na sheria ni kule kutumiwa kwa vipaza sauti na wanawake kwa kuimbia wakati wa harusi na sauti hizo kuwafikia wanaume walioko nje ya sehemu hiyo. Lakini hapana makosa iwapo watatumia vipaza sauti hivyo lakini vikasikika kati ya wao kwa wao.

Na jambo lengine ni la kupigwa kwa picha kwa wanawake ama kuchukuliwa kwa kanda la video. Hilo halina makosa iwapo picha hizo ama kanda hizo za video hazitaangaliwa na wanaume wa kando.

Hakika ukosefu wa kuchungwa sheria za dini katika mambo kama haya hakusababishi madhambi tu, bali hupelekea hata katika matatizo ya kijamii na tabia.

**Kuwachosha maharusi wawili**

Inatakiwa kuwe na utulivu kwa maharusi wawili ili wasichoke na kuweza kuutia usiku wao wakiwa wachangamfu kiroho na kimwili. Lakini ukweli ni kwamba maharusi hawa huchoshwa kwa kuwepo kwa shughuli na mambo mengi wakati wa harusi kama vile bibi harusi kupelekwa saloon na kutumia zaidi ya masaa matatu ama matano ili kutengenezwa nywele kisha atumie zaidi ya masaa

mawili katika studio kupigwa picha, kisha awe kwa tena saa moja ama mawili kulingana na rtatiba za harusi na pengine akifika kwa mume wake na baada ya masaa sita kwa uchache na wakati mwengine hata masaa kumi hali ya kuwa amechoka kimwili na akili.

Na vile vile kwa bwana harusi lakini huwa ni afadhali kidogo. Basi kuwachosha maharusi kwa njia hizi huwa zi uzuri na kuleta madhara wakati mwengine. Na nimechunguza katika kiafya mtu huweza kupatwa na maradhi ya pumzi, mafua, ama machovu ya hali ya juu.

**Ndoa ya jumuia**

Hivi punde tu kumedhihiri katika jamii yetu jambo zuri na kigezo chema nalo ni kuanzishwa kwa kamati katika kila sehemu zinazohusika na usimamizi wa mambo ya harusi katika sehemu hiyo kamati hizo zinajiita sherehe ya ndoa ya jumuia.

Na wanaandaa usiku maalumu na kushuhulika na kueneza uwalishi na kutayarisha mahali penye nafasi na kuandaa chakula cha harusi kisha wanakusanyika maharusi wote pamoja wakiwemo jamaa na vijana wa mjini. Kisha huweko na shughuli mbali mbali kama vile mawaidha, qasida na baadhi ya mashairi, kisha wanashikanishwa maharusi na jamii yote hubaki na furaha na uchangamfu kwa jumla.

Katika shughuli hii kila maharusi hutowa kiwango fulani cha pesa na kukabidhi kamati simamizi kwa ajili ya matayarisho hayo. Wenye harusi uhudhuria kama wageni tu hawasimamii jambo lolote bali kuila kitu kinafanywa na kusimamiwa na kamati hizo.

Basi kamati hizi zinapaswa kutiliwa nguvu na tusiwe na mawazo mabaya dhidhi yake. Na kusiwe na mawazo kwamba wenye harusi hawajisikii kama wahusika na mengineyo. Haya ni mawazo yanayoinyima jamii faida kubwa na kuleta hali ya kubaguana.

Sheikh Hassan bin Musa bin bin Sheikh Ridha Saffar, amezaliwa mnamo mwaka (1377 A.H.) huko mjini Qatif, Mkoa wa Mashariki, nchini Saudi Arabia. Alipohitimu kusoma katika Chuo cha Qur'an, alijiunga na Madrasa ya msingi ya Zainul-Abidin, kisha akajiunga na Madrasa ya Kati ya Amin mjini Qatif, na hivyo kuanza kutoa khutba za kidini katika mwaka 1388 (A.H.) (1968 A.D.).....................................................

Mnamo mwaka 1391 (A.H.) (1971 A.D.), alikwenda huko mjini Najaf, Iraq kwa ajili ya kuongeza elimu na baadaye alikwenda kuendelea zaidi kwenye Hawza ya Qum (Iran).

Kisha alijiunga na Madrasa ya Rasuulul-Akram nchini Kuwait, na hapo ndipo alipokuwa ni miongoni mwa viongozi wa mwamko wa kiislamu nchini humo.............................

Sheikh Saffar amesimamia taasisi nyingi za kidini katika pande nyingi duniani ikiwemo Saudia, Oman, Syria, Iran na Marekani..........................................................

Vilevile ameshiriki katika matangazo mengi kupitia kwenye idhaa na magazeti mengi duniani. Ameshiriki mikutano mingi ya kiislamu ikiwemo Mkutano wa vijana wa kiislamu Marekani, na mkutano wa Umoja wa kiislamu chini Iran, pia vikao juu ya fikra katika Saudia; pia mkutano wa mlingano wa ....... kuwa karibu baina ya madhehebu, nchini Bahrain.......................................

Ametoa vitabu zaidi ya sabini na vimetarumiwa katika lugha mbali mbali za kigeni...........................................................................

Sheikh huchukuliwa kama ni mmoja kati ya watu.......... wanaopenda kuzungumzia uhuru wa kuwapo kwa wingi wa kiitikadi, na juu ya uelewa wa uzalendo na pia kufikia kuwa na neno moja katika Uislamu.